Namba ya Mtahiniwa _____

Jina la shule: _____

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA WAZIRI MKUU TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA JIJI LA DAR ES SALAAM

MTIHANI WA UTAMILIFU WA KATA

DARASA LA SABA - MACHI, 2026

01 KISWAHILI

Muda: Saa 1:40 **Tarehe: .....**

MAELEKEZO

1. Karatasi hii ina sehemu A, B na C zenye jumla ya maswali Sita (6)
2. Jibu maswali **yote** katika nafasi uliyopewa.
3. Majibu yote yaandikwe katika karatasi hii.
4. Majibu yote yaandikwe kwa kalamu yenye wino wa bluu au mweusi.
5. Simu za mikononi na vifaa vingine visivyohitajika haviruhusiwi katika chumba cha mtihani.
6. Andika kwa usahihi **Namba yako ya Mtihani na Jina la Shule** kwenye sehemu ulizopewa.

KWA MATUMIZI YA MTAHINI TU		
Namba ya Swali	**Alama**	**Saini ya Mhakiki**
1		
2		
3		
4		
5		
6		
Jumla		

SEHEMU A: (Alama 20)

1. Sikiliza kwa makini habari utakayosomewa na Msimamizi kisha jibu kipengele cha (i) – (v) kwa kuchagua herufi ya jibu sahihi.

(i) Kanju na wenzake walipanga kwenda kuvunja duka la nani?

(a) Mangi (b) Shule (c) Kijiji (d) Mtaa (e) Mzee Hekima [ ]

(ii) Baada ya wahakijiji kuwakamata Kanju na wenzake walitaka kuwafanya nini?
(a) Kuwasamehe (b) Kuwalipisha fidia (c) Kuwapeleka kituo cha polisi
(d) Kuwachoma moto (e) Kuwachapa viboko [ ]

(iii) Nani aliyeokoa jahazi kwa kuwasihi wanakijiji wasiwachome moto Kanju na wenzake?
(a) Wanakijiji (b) Polisi (c) Mzee Hekima
(d) Kanju (e) Mahakama [ ]

(iv) Methali iliyojitokeza katika habari uliyosikiliza ni ipi?
(a) Omba radhi (b) Sheria ni msumeno (c) Tia mkononi
(d) Okoa jahazi (e) Ponda mali [ ]

(v) Kanju na wenzake walihukumiwa kifungo cha miaka mingapi kila mmoja ?
(a) Miwili (b) Kumi (c) Sita (d) Saba (e) Mitano [ ]

2. Chagua herufi ya jibu sahihi katika kipengele i - x

(i) Wanafunzi wote walipanga vitabu vyote kabatini. Neno **kabatini** limetumika kama aina gani ya kielezi?
(a) namna (b) kuonesha (c) mahali (d) idadi (e) wakati [ ]

(ii) Katika vitenzi **sitakula** na **hushibi** ni silabi zipi zinaonesha ukanushi?
(a) si na shi (b) ja na bi (c) ku na hu
(d) ta na shi (e) si na hu [ ]

(iii) Askari kanzu amemkamata mwizi. Sentensi hii imetumia mtiririko upi wa aina za maneno?
(a) N+N+T+V (b) N+W+T+E (c) N+V+T+N
(d) N+N+T+E (e) W+N+T+V [ ]

(iv) Kunguru hafugiki kwa sababu anapenda kuokota majalalani. Sentensi hii ipo katika kauli gani ya utendaji ?
(a) kutenda (b) kujitendea (c) kutendeana
(d) kutendeka (e) kutendekana [ ]

(v) Kiranja Mkuu wa shule _____ mawazo ya wanafunzi wenzake katika kikao cha uongozi wa shule. Neno lipi linakamilisha sentensi hiyo?
(a) aliwakilisha (b) ariwasilisha (c) aliwasilisha
(d) aliwasilishwa (e) hakuwakirisha [ ]

(vi) Mambo mema na mabaya hayafungamani. Kifungu hiki cha maneno kinatoa maana ya methali ipi kati ya zifuatazo?
(a) Gongo la mbuyu si la mvule (b) Liwapo lako ni jema la mwenzio ni baya
(c) Lila na fila havitangamani (d) Padogo pako si pa kubwa kwa mwenzako
(e) Simba mwenda pole ndio mla nyama [ ]

(vii) Jumanne alipumzika chini ya mti. Alipoulizwa anafanya nini hapo. Alijibu **anavinjari**. Nini maana ya neno lilikorezwa?
(a) Napiga domo (b) Napunga upepo (c) Napiga kambi
(d) Nimepigwa na butwaa (e) Nazunguka mbuyu [ ]

(viii) Uzi mwembamba umefunga dume kubwa. Upi ni jibu la kitendawili hiki?
(a) Mawingu (b) ndoto (c) mvua (d) ugonjwa (e) usingizi [ ]

(ix) Mkutano haukufanyika kwa sababu Mwenyekiti na Katibu hawakufika. Kifungu kipi cha maneno kati ya vifutavyo kinasadifu sentensi hiyo?
(a) Mkutano uliarishwa (b) Mkutano ulahirishwa (c) Mkutano ulihairishwa
(d) Mkutano ulihairishwa (e) Mkutano ulihairishwa [ ]

(x) Panya huyu anakula unga wangu. Wingi wa sentensi hii ni upi?
(a) Panya hawa wanakula unga wangu. (b) Mapanya hawa wanakula unga wetu.
(c) Panya hizi zinakula unga zetu. (d) Panya hawa wanakula unga wetu.
(e) Panya hizi zinakula unga wetu. [ ]

3. **Oanisha maneno ya yaliyopo katika orodha A na maelezo yaliyopo orodha B kwa kuandika herufi ya jibu sahihi katika nafasi ya jibu.**

Orodha A			Orodha B	
(i)	Kaka	[ ]	A.	Mchanganyiko wa vitu au mambo mbalimbali
(ii)	Mseto	[ ]	B.	Vaa miwani
(iii)	Piga maji	[ ]	C.	Ganda la kiberiti
			D.	Mtoto wa meza
(iv)	Kitate	[ ]	E.	Tui la nazi
			F.	Maneno yenye sauti zinazokaribiana kufanana katika matamshi.
(v)	Saraka	[ ]	G.	Maneno yenye maana sawa.

SEHEMU B: (Alama 20)

4. **Andika majibu sahihi katika sehemu zilizoachwa wazi.**

(i) Sentensi iliyokamilika huundwa na kitenzi. Kitenzi huonesha nyakati kutokana na mofimu zilizopachikwa katika mzizi wa kitenzi. Je, katika sentensi ifuatayo ni mofimu ipi inaonesha wakati? **Juma hachezi mpira.** _____

(ii) Lipi ni jibu la kitendawili kifuatacho? Anachora lakini hajui achoracho. Jibu liwe na silabi mbili tu _____

(iii) Mama anapika, baba analima na dada anacheza mdako lakini mimi ninachota maji kisimani. Sentensi hii ina viunganishi vingapi? _____

(iv) Mahali ambapo hutumika kutengeneza magari yaliyoharibika na mahali ambapo hutumika kutengeneza samani huitwa kwa jina moja. Je, ni jina gani hilo?

_____

(v) Kutohoa ni njia ya kuchukua maneno kutoka katika lugha moja na kuingiza katika msamiati wa lugha nyingine. Neno papai ni la Kihispania. Je, neno shati limetoholewa kutoka kwenye lugha gani? _____

5. **Soma shairi lifuatalo kwa makini kisha jibu maswali yanayofuata**

Baragumu napuliza, lipo jambo linakera,
Wote mlosikiliza, wazee hata kapera,
Kwa makini sikiliza, hali hii si bora,
Jambo lenyewe ugonjwa, UKIMWI jina nataja.

Maswali

(i) Janga linalozungumziwa katika shairi hilo ni UKIMWI . Andika kirefu cha janga hilo.

_____

(ii) Andika mleo wa shairi hilo _____

(iii) Neno 'kapera' kama lilivyotumika katika shairi lina maana gani?_____

(iv) Msanii anaposema hali sio bora ana maana gani? _____

(v) Mshairi ametunga shairi lake kwa ustadi. Je, ametumia muundo gani?

_____

SEHEMU C: (Alama 10)

6. Soma kwa makini habari kisha majibu maswali

Ufisadi ni hali ya kutenda mambo ambayo yanakwenda kinyume na sheria na maadili mema. Msukumo mkuu wa ufisadi ni ubinafsi. Mtu huongozwa na matamanio ya moyo wake. Hutenda mambo ambayo yanamfaidisha yeye binafsi bila kuwazia kama yatasaidia jamii yake au la. Matendo ya ufisadi yanahusu mambo kama unyakuzi na wizi wa mali ya umma. Watu hutumia vyeo kujitajirisha na kupendelea jamaa au watu wa kabila lake. Kiongozi kama huyu anasahau kuwa uongozi ni dhamana kubwa anayopewa mtu kwa faida ya umma. Ufisadi unaweza kuwa chanzo cha kudumaa kwa maendeleo. Mali zinafujwa na viongozi, huduma kama vile hospitali, shule na miundombinu hukwama kutokana na ufisadi huo. Ukosefu wa huduma hizi husababishwa na kuzorota kwa uchumi.

Maswali:

(i) Ufisadi ni nini?_____

(ii) Mwandishi anasema kuwa viongozi walifuja mali kutokana na ufisadi. Nini maana ya kufuja mali?_____

(iii) Kiongozi anayetenda ufisadi anasahau kuwa uongozi ni dhamana kubwa anayopewa mtu kwa faida ya nani?_____

(iv) Huduma za hospitali, shule na miundombinu mbalimbali hukwamishwa na nini?

_____

(v) Kwa mujibu wa kifungu cha habari ulichosoma, matendo ya ufisadi yanahusu mambo gani?_____

MTIHANI WA UTAMILIFU WA KATA

MAELEKEZO KWA MSIMAMIZI KATIKA UPIMAJI WA UJUZI WA KUSIKILIZA, (SWALI LA i-v)

01 KISWAHILI **UJUZI WA KUSIKILIZA**

Soma kimya maelekezo ya msimamizi Sehemu ya Kwanza na baada ya hapo soma kwa sauti na kwa umakini maelekezo kwa watahiniwa katika Sehemu ya Pili. SEHEMU YA KWANZA

Maelekezo kwa Msimamizi

1. Soma hadithi kwa sauti na kwa umakini.
2. Waeleze watahiniwa kuwa utasoma hadithi mara mbili, hivyo kila mmoja asikilize kwa umakini.
3. Waeleze watahiniwa kuwa ukisoma hadithi kwa mara ya kwanza, wasikilize bila kujibu maswali na ukimaliza kusoma mara ya pili wajibu swali la 1-5 katika karatasi maalum kisha wataendelea kujibu maswali mengine kwenye karatasi hiyo.
4. Soma hadithi taratibu kwa mara ya kwanza huku ukizingatia alama zote za uandishi zilizopo katika hadithi hiyo. Unaposoma kwa mara ya pili ongeza kidogo kasi ya usomaji.
5. Muda utakaotumika kwa msimamizi kusoma hadithi ni dakika tano (05), pia muda utakaotumika kwa watahiniwa kujibu maswali ni dakika tano (05). Sehemu hii itafanyika kwa dakika kumi (10).

SEHEMU YA PILI

Maelekezo ya Msimamizi kwa Watahiniwa

1. Nitasoma hadithi kwa sauti.
2. Nitasoma hadithi mara mbili, hivyo kila mmoja asikiize kwa umakini.
3. Nitakaposoma hadithi kwa mara ya kwanza, unapaswa kusikiiza. Nikimaliza kusoma mara pili utajibu maswali.
4. Utatumia muda wa dakika tano (05) kujibu swali 1-5 kisha utaendelea kujibu maswali mengine (6-45).

NB

HADITHI

Kanju na wenzake walipanga kwenda kuiba dukani kwa Mangi. Wanakijiji waliwakamata na kutaka kuwachoma moto, lakini Mzee Hekima aliokoa jahazi. Mahakama iliwaweka jela miaka mitano kila mmoja kwani sheria ni msumeno, hukata mbele na nyuma..